



## Kujifunza Kupitia Kucheza katika Mazingira ya Utotonii

KISWAHILI

### Mchezo ni nini?

Tafiti ulimwenguni kote zimeonyesha kuwa watoto hujifunza na kukua wakati wanaposhiriki katika matukio muhimu ya michezo.

*"Mchezo ni muhimu ili kuchocha na kuunganisha uwezo anuwai wa kiakili, kimwili, kijamii na ubunifu wa watoto. Mazoezi madhubuti ya utotoni hutumia mbinu jumuishi za ufundishaji na ujifunzaji ili kusaidia mwingiliano endelevu na wa pamoja na watoto. Kupitia mchezo na fursa nynginezo watoto hujifunza kuelewa na kujenga mawazo kuhusu ulimwengu wa kijamii na asilia, watu, mahali, vitu na matukio wanayokutana nayo kila siku."*

- VEYLDF, 2016, pg. 14

Kucheza kunakuja kwenyewe kwa mtoto wako na ni sehemu muhimu ya kujifunza na kukua kwake. Kucheza humsaidia mtoto wako kuelewa ulimwengu wake na kuendelea kustawisha utambulisho thabiti. Kupitia mchezo mtoto wako anaweza kufikiria, kujifanya, kuunda, kugundua, kuchunguza, kuwasiliana, kuuliza, kuzungumza, kusikiliza, kufikiri, kuhisi, kugusa na kunusa. Mchezo huhusisha kuhawilisha, kutatua matatizo, kujihatarisha, kujaribu mambo mapya, na kuona jinsi mambo yanavyofanya kazi. Mtoto wako atajifunza kuhusu yeye mwenyewe na wengine, kujifunza kanuni za mchezo, kuwa na marafiki, kuendeleza mahusiano na kuwaamini watu walio karibu yake ikiwa ni pamoja na waelimishaji wake na watoto wengine.

Wakati mwingine watoto watacheza peke yao, watacheza na mtoto mmoja au wawili na watacheza katika vikundi vidogo au vikubwa vyta watoto. Mchezo unaweza kuwa wa kelele au tulivu, wa kukaa tu au wa kujishughulisha.

*"Vipindi vyta michezo ya bila kukatizwa huropa watoto wasaa wa kuvumbua, kuchunguza na kugundua, kwa kutumia vifaa na nyenzo nyngi zisizo wazi."*

- VEYLDF, 2016, pg. 21

### Kujifunza kupitia mchezo

Walimu na waelimishaji hupanga mpango ili kukidhi maslahi na mahitaji ya kila mtoto anayehudhuria kwenye huduma. Wanafanya hivi kwa kutoa matukio mbalimbali yaliyojikita kwenye michezo katika mazingira ya wazi ya kujifunzia, ambapo watoto wanaweza kutembea kwa uhuru kwenye sehemu za ndani na nje.

Kutakuwa na shughuli rasmi zilizolekezwa, kama vile muziki, hadithi na mijadala. Kwa sehemu kubwa ya siku, watoto watakuwa wakifanya maamuzi peke yao kuhusu wapi wacheze, wacheze na nani, na muda gani watumie kwenye mchezo husika. Waelimishaji watatoa usaidizi na mwongozo watoto wanapohitaji msaada.

Waelimishaji watatumia mbinu mbalimbali za ufundishaji kuwasaidia watoto kukuza upendo wa kujifunza, kuwa wadadisi, kuuliza maswali na kupendezwa na ulimwengu wao na watu wanaokutana nao. Wanaweza kuongoza mchezo, kuongoza igizo, au kuangalia watoto katika mchezo wa kujiongoza wenywewe.

## Je, watoto wanajifunza nini wakati wa kucheza?

Mchezo huwapa watoto fursa ya kuzungumza na kuuliza maswali, kukuza na kufanya mazoezi ya msamati na lugha, kusoma na kuandika, kuhesabu na stadi za kijamii. Kupitia mchezo, watoto wanajifunza jinsi ya kuwasiliana na kuhusiana na watu wengine.

Pia watoto hutumia mawazo yao kuigiza yale waliyoyaona, kwa mfano;

- Kujifanya wanaanda chakula
- Wanamtunza mtoto
- Kuwa mzima moto, daktari au muuza duka.

Hii huwasaidia watoto kujifunza kuelewa na kufahamu ulimwengu wao na jamii yao.

*"Mchezo wa kuigiza ni muhimu kwa ajili ya kugundua utambulisho na mitazamo tofauti, ikiwemo dhana ya kuwa wa sehemu ya jumuiya za kimataifa. Watoto wanapaswa kuungwa mkono ili kukubali ufanano na utofauti kati ya watu binafsi na vikundi, na kuheshimu mitazamo tofauti."*

- VEYLDF, 2016, pg. 18

Mtoto wako anaposhiriki katika mchezo, atajadili kuhusu kanuni ili kumsaidia kujifunza tabia zinazokubalika kwa wengine. Kwa mfano, watoto wanaweza kuunda kanuni za kusubiri zamu yao kwenye bembea. Kuwaruhusu watoto kushiriki katika kutunga kanuni zinazomsaidia kila mtu kukaa salama, kutunza vifaa na kuunga mkono haki na usawa, kutasaidia ujuzi wao wa kufikiri na kutatua matatizo, na kutasaidia maendeleo yao ya mawasiliano na ujuzi wa kijamii pamoja na ujuzi wao wa kuhesabu na kusoma na kuandika.

Katika mchezo wao, watoto wanaweza kujenga kwenye ujuzi na mawazo yao yaliyopo kwa njia mpya na za kuvutia.

Watoto wanaweza kurudia baadhi ya shughuli tena na tena, wakijiweka kwenye hatari na kujifunza na kufanyia mazoezi maarifa, kama vile;

- kupanda sehemu ya juu wao wenyewe
- kuelewa fumbo la jig-saw
- kuвая nguo zao wenyewe au gwanda la sanaa
- kuweka ulingano kwenye boriti nyembamba
- kutumia mkasi wao wenyewe
- kuruka kwa mguu mmoja
- kujisukuma wenyewe kwenye bembea.

Mafanikio haya, makubwa na madogo, ni zawadi kwa watoto, familia zao na kwa waelimishaji wanaosaidia kujifunza kwao.

Mchezo huwapa watoto fursa ya; kushereheke, kufanikiwa, kufaulu, kufanya makosa, kufanya mazoezi, kujaribu taarifa au ujuzi mpya, kutengeneza maoni na kufahamu ujuzi na maarifa mapya.

Mchezo ndiyo jinsi mtoto wako anajifunza.

### Marejeo

Department of Education and Training, 2016. *Victorian Early Years Learning and Development Framework*.